END TB

JINSIA NA KIFUA KIKUU

eannaso

NTLP NATIONAL TUBERCULOSIS & LEPROSY PROGRAMME

Tanzania TB Community Network

Stop TB Partnership hosted by UNOPS

JE, JINSIA INAUHUSIANO NA MAPAMBANO DHIDI YA KIFUA KIKUU?

Tunaweza kusema kuwa jinsia ni jambo jipya katika mapambano dhidi ya Kifua Kiku. Lakini Kifua Kikuu kimekuwa chanzo kikubwa cha vifo vya wanawake duniani. Kuna hitaji la dharura kuelekeza nguvu na rasilimali ili kutambua ni kwa namna gani hatari za maambukizi ya Kifua Kikuu na athari zake zinachangiwa na jinsia na mambo ya kijinsia. Kwa kutambua changamoto hii, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu, na Malaria (Global Fund) na Washirika wa Kuzuia Kifua Kikuu wanaelekeza uzingatiaji wa jinsia katika kupambana na VVU, Kifua Kikuu na Malaria. Pia, kupitia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), serikali zimeahidi kutimiza malengo kadhaa yanayohusiana na usawa wa kijinsia na afya, ikifuatana na malengo ya kutokomeza Kifua Kikuu, na kutoa takwimu iliyogawanywa kwa kuzingatia jinsia kuhusu Kifua Kikuu (Lengo 3.3), na pia kwa magonjwa yasiyoweza kuambukiza ambayo huchangia vifo vinavyohusiana na Kifua Kikuu (Lengo 3.4).

NI KWA NAMNA GANI JINSIA INAHUSIANA NA MAPAMBANO DHIDI YA KIFUA KIKUU?

Kulingana na Shirika la Afya Duniani (WHO), wanaume ulimwenguni wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa na kufa kutokana na Kifua Kikuu kuliko wanawake. Tazama Kielelezo Na. 1.



Kielelezo 1. Viwango vya Kifua Kikuu ulimwenguni Mwaka 2018.

Ingawa kuna wanawake wengi wanaoishi na VVU katika Jangwa la Sahara Kusini mwa Afrika, maambukizi ya Kifua Kikuu ni makubwa kwa wanaume kuliko wanawake, isipokuwa tu kwa wasichana walio kwenye umri wa kuvunja ungo, pamoja na wanawake wenye umri wa miaka 15-25 wanaoishi katika mwaeneo yenye maambukizi makubwa ya VVU. Hatahivyo, Ugonjwa wa Kifua Kikuu unaweza kuwa na athari mbaya zaidi kwa wanawake, hasa katika umri wa uzazi na wakati wa ujauzito. Huduma za afya ya mama na mtoto zina mkakati thabiti wa kutoa huduma za Kifua Kikuu pale tu wanapoanza kupata huduma za kliniki ili kuongeza huduma kwa wanawake na familia zao.

NI MAMBO GANI HUSABABISHA KUWEPO KWA TOFAUTI ZA KIJINSIA KATIKA UGONJWA WA KIFUA KIKUU?

WANAUME

- Mwingiliano mkubwa kijamii
- Wengi wao hufanya kazi katika maeneo hatarishi zaidi
- Wengi wao hutumia sigara
- Wengi wao hutumia vilevi
- Mara nyingi matibabu yao huathiriwa na uhamaji wa mara kwa mara kwaajili ya kazi

WANAWAKE

- Hukumbwa na unanyapaa zaidi
- Ni wahudumu wakubwa wa familia; hivyo, wanakuwa katika hatari zaidi ya kuambukizwa
- Dalili za Kifua Kikuu huchelewa kuonekana kwa wanawake
- Ufikiaji duni wa huduma za afya
- Ufikiwaji mdogo wa taarifa zinazohusu Kifua Kikuu
- Wengi huathiriwa na Kifua Kikuu cha nje ya mapafu; hivyo, kuna ugumu wa kuwapima na kugundua maambukizi

Huduma za kukabiliana na Kifua Kikuu zinahitaji kuzingatia tofauti hizi ili kufanikisha mapambano dhidi ya Kifua Kikuu. Mambo ya kijinsia katika mapambano dhidi ya Kifua Kikuu, matibabu na viwango vya wanaopona vinatofautiana duniani. Katika nchi nyingine, wanaume wana matokeo bora kuliko wanawake, wakati katika nchi nyingine wanawake ndio wana matokeo bora. Kwenye nchi nyingi zenye kipato cha chini na cha kati, theluthi mbili ya matukio ya Kifua Kikuu yaliyoripotiwa ni wanaume na theluthi moja ni wanawake, na haieleweki vizuri ni kwa nini kuna tofauti hizi.

JE, KUNA VIKWAZO GANI VYA KIJINSIA KATIKA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA KIFUA KIKUU

Ingawa wanaume wanakabiliwa na hatari kubwa ya kuambukizwa na kufa kutokana na Kifua Kikuu, wanawake wanaweza kuwa na ufikiaji mdogo wa matibabu ya Kifua Kikuu na kinga dhidi ya Kifua Kikuu kuliko wanaume. Katika mazingira mengine, kuna uwezekano mdogo kwa wanawake kupata vipimo vya makohozi.

Wanaume kutokuwa tayari kulipia huduma za afya kwa wanawake. Afya wa mwanamke kuonekana haina umuhimu kama vile afya ya mwanaume, au kwasababu wanawake wenye Kifua Kikuu wananyanyapaliwa kuliko wanaume. Katika maeneo mengine, unyanyapaa na kubaguliwa kunaweza kuwa wanawake wenye Kifua Kikuu wanachukiwa na familia zao pamoja na jamii.	Wanawake huchukua muda mrefu kupata vipimo na matibabu ya Kifua Kikuu, jambo ambalo hufanya wengine wakate tamaa ya kutafuta huduma kutokana na kutokuwepo kwa usiri pamoja na kukosekana kwa sehemu za kuhudumia watoto katika vituo vya afya wanavyoenda kutafuta matibabu.	Wanawake walio magerezani wana uwezekano mkubwa wa kukosa huduma za matibabu ya Kifua Kikuu kuliko wanaume gerezani.

JE, NI MAMBO GANI YANAWEZA KUWA MFANO WA MWITIKIO WA KUONDOA TOFAUTI ZA KIJINSIA?

Ikiwa muda wa kufanya kazi kwa wanaume (au wanawake) unazuia kutafuta huduma za afya, hatua muhimu zinaweza kujumuisha huduma za simu, kuongeza bajeti, kuwa na saa nyingi ya huduma katika vituo vilivyowekwa, viongozi wa jamii, vikundi vya wanaume na wanawake, pamoja na wadau wengine kuhamasisha watu wajue umuhimu wa ufikiaji wa huduma kwa wote. Ikiwa wanaume hawatumii huduma za msingi za afya kwa sababu zinaonekana kuwepo kwa ajili ya wanawake na watoto, kwa mfano, uhamasishaji unaweza kubadilisha mitazamo.

Kama wanaume wanaathirika zaidi na Kifua Kikuu kwasababu ya kuhamahama kwaajili ya kazi, uhamasishaji unaowalenga wanaume unaweza kuleta mafanikio.

Katika maeneo yaliyo na maambukizi mengi ya VVU, huduma za Kifua Kikuu na taarifa zinapaswa kutolewa kwa wanawake wanaotafuta utunzaji wa VVU na msaada katika kuzuia maambukizi ya VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto. Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) unapendekeza mfumo wa ushirikiano miongoni mwa watoa huduma za Kifua Kikuu, VVU, na huduma ya afya ya mama na mtoto ili kufisha taarifa na huduma za Kifua Kikuu kwa wanawake.

Barani Africa, viwango vya maambukizi ya Kifua Kikuu ni mara 10 zaidi kwa wanawake wajawazito wenye VVU kuliko wanawake wajawazito wasio na maambukizi ya VVU (WHO, 2018).

TUNAHITAJI KUFANYA TAFITI GANI?

TAFITI JUU YA JINSIA NA KIFUA KIKUU ZINAHITAJI KUWA NA MWELEKEO UFUATAO:

- Kubainisha ukubwa wa tofauti za kijinsia katika mambo yanayohusiana na Kifua Kikuu, kuanzia pale maambukizi yalipotokea mpaka kupona pamoja na kujenga na kurejesha mwili katika afya yake kwa kuanza na:
  a) Kuhakikisha kwamba takwimu mpya kuhusu maendeleo ya taifa katika mapambano dhidi ya Kifua Kikuu zinachambuliwa kwa kutofutisha jinsia na makundi ya kiumri, na
  b) kupitia upya takwimu za tafiti zilizofanyika zamani, pamoja na takwimu za programu ya Kifua Kikuu ili kuzipanga kwa kuzingatia jinsia na makundi ya kiumri.
- Kuchunguza sababu zinazochangia tofauti za kijinsia ili kubaini ni kwa kiasi gani zinachangiwa na tofauti za kibaolojia, kijamii/ kitamaduni au zinasababishwa na mwajiri kwa kulinganisha matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanyika katika maeneo tofauti.
- Kuchunguza ni kwa namna gani hasa Kifua Kikuu huwaathiri wanawake walio katika umri wa kuzaa, haswa afya zao za uzazi, pamoja na afya ya mtoto akiwa tumboni na baada ya kuzaliwa.

JE, NI UTEKELEZAJI GANI WA KISERA NA PROGRAMU YA KIFUA KIKUU UNAHITAJIKA?

- Programu ya kudhibiti ugonjwa wa Kifua kikuu inahitaji kukuza elimu sahihi ya afya juu ya dalili za Kifua Kikuu, utambuzi na matibabu kwa jamii na wahudumu wa afya, ili kupunguza kuchelewa matibabu. Tofauti za kijinsia zinazoathiri tabia ya kutafuta huduma za afya na mwitikio baada ya kugundua maambukizi ya Kifua Kikuu lazima ziingizwe katika programu za elimu ya afya.
- Kampeni za kuhabarisha wanajamii zinahitajika ili kufanya wajue ni wapi matibabu sahihi ya Kifua Kikuu yanapatikana ili wasiende kupata matibabu ya Kifua Kikuu kutoka kwa watu au watoa huduma wasio na utaalamu au sifa. Kampeni kama hizo zinapaswa kulenga wanawake, vijana, na makundi mengine ya kijamii yalivyo katika hatari zaidi.
- Usimamizi wa jamii au mfumo wa usimamizi katika familia uangalizi wa usimamizi wa serikali, upimaji, utumiaji wa dawa kwa miezi kati ya sita na tisa chini ya uangalizi ya mhudumu wa afya (DOTS) angalau kwa miezi miwili ya mwanzo na ufuatliliaji ili kuhakikisha matibabu yamefanikiwa unaweza kufanikisha matibabu na matokeo chanya miongoni mwa wanawake na wanaume ambao hawawezi kufika kwenye vituo vya matibabu kila siku.
- Kuingizwa kwa maswala ya kijinsia katika mitaala ya mafunzo kwa watoa huduma na wasimamizi wa programu ya Kifua Kikuu.

TUTATAONDOAJE VIKWAZO VYA KIJINSIA KATIKA HUDUMA ZA KIFUA KIKUU?

Kwanza, nchi inahitaji kuelewa idadi ya watu walio katika hatari ya kuambukizwa Kifua Kikuu na wanaoishi na Kifua Kikuu ambao wanaweza kuwa, kwa mfano, wanaume walio hatarini. Tathmini ya vikwazo vya kijinsia katika upatikanaji wa huduma katika jamii fulani na ukusanyaji wa takwimu za Kifua Kikuu zinazozingatia jinsia, ukubwa wa maambukizi na upatikanaji wa huduma zitazaidia kupanga mipango ya kufikia makundi ya wanaume na wanawake, mafunzo kwa wafanyakazi wa afya pamoja na mipango mingine ya kuboresha afya.

Tathmini zinazozingatia jinsia zitabainisha kanuni, sera na sheria pamoja na mikakati ya kiutekelezaji iliyoshidwa kuondoa vikwazo vya kijinsia katika upatikanaji wa huduma.

TATHMINI YA JINSIA KATIKA KUKABILIANA NA KIFUA KIKUU INCHINI TANZANIA

Zana ya kufanya tathmini ya jinsia katika kukabiliana na VVU na Kifua Kikuu imeandaliwa na Programu ya Pamoja ya Umoja wa Mataifa juu ya VVU / UKIMWI (UNAIDS), washirika wa kutokomeza Kifua Kikuu (STOP TB Partnership) na Mfuko wa Dunia (Global Fund) kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO), mashirika ya kijamii, na wataalamu wa Kifua Kikuu.

Zana hii sio tu inasaidia nchi na uwasilishaji wa ombi la ufadhili wa kijinsia kwa Mfuko wa Dunia lakini imekusudiwa kusaidia nchi kutathmini muktadha wa janga la VVU na Kifua Kikuu na mtazamo wa kijinsia, kuwasaidia kutekeleza afua ambazo zinazingatia jinsia ili kupunguza maambukizo ya VVU na Kifua Kikuu. Hii imekusudiwa kufanya kazi katika maeneo ya maambukizo ya UKIMWI na Kifua Kikuu kama tathmini moja ya pamoja au pia inaweza kufanywa kwa kila ugonjwa kitofauti.

Ili kutekeleza mahitaji haya mathubuti, Mwaka 2017, Tanzania ilifanya tathmini ya Jinsia katika Kukabiliana na Kifua Kikuu na UKIMWI ambayo iliongozwa na wataalamu Mitandao ya Kitaifa ya Jumuiya za Huduma za Afya na Ukimwi Afrika Mashariki (EANNASO). Kusudi la tathmini hiyo lilikuwa ni kubainisha uzingativu wa masuala yahusuyo jinsia katika mapambano dhidi ya VVU na Kifua Kikuu nchini Tanzania kuanzia kwenye hatua za upimaji hadi matokeo ya matibabu. Hii iliangalia mwitikio wa mapambano dhidi ya VVU na Kifua Kikuu kwa mtazamo wa kijinsia na kutoa mapendekezo ya kuboresha mwitikio wa Kifua Kikuu ili kutoa huduma bora za Kifua Kikuu zinapatikana na kukubalika kwa wote. Mapendekezo haya yametumika kuandaa Mpango wa Kitaifa wa Haki ya Jamii na Jinsia ili kuokoa maisha ya watu wengi, kuboresha afya zao, maisha bora kwa wanawake na familia zao ili kutekeleza Haki ya Jamii na kubainisha mambo ambayo yanaweza kuathiri usawa wa kijinsia nchini Tanzania.

MAREJEO MUHIMU

EANNASO, STOP TB – Gender Assessment of the National Response To TB in Tanzania
Stop TB – The Global Plan 2016-2020
Global Fund -Technical Brief on TB, Gender and Human Rights
Measure Evaluation – The Importance of Gender in Tuberculosis Data
Stop TB and UNAIDS -TB/HIV Gender Assessment Tool
UNDP- Gender and TB Discussion Paper
W4GF – Webinar: TB and Gender Assessments
World Health Organization – Tuberculosis in Women

NOTE

WASILIANA NA NASI

Tanzania TB Community Network (TTCN)

Hosted by EANNASO

Plot # 1 Olorien, Kijenge | Off Njiro Road

P.O Box 6187 | Arusha, Tanzania

+255 739 210598 ttcn.tanzania@gmail.com ttcntanzania

END TB

Tanzania TB Community Network